**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI TANZANIA

## SHULE YA SEKONDARI BONYOKWA

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU– TAMISEMI**

**SHULE YA SEKONDARI BONYOKWA**

Namba za simu;
Mkuu wa Shule +255 (0) 755865326
Makamu Mkuu wa Shule +255 (0) 714057027
Mtaaluma mkuu +255 (0) 0714333431
**Barua pepe:**
bonyokwasecondaryschool@gmail.com

S.L.P 24302,
**DAR ES SALAAM**.

Tarehe…………………………….

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ………….**
**……………………………………………..**
**S.L.P …………………………………..**
**…………………………………………….**

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI BONYOKWA HALMASHAURI YA JIJI LA DAR ES SALAAM MKOA WA DAR ES SALAAM MWAKA .......................**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka .......................na atasoma tahasusi ya ……………..

Shule ya Sekondari **BONYOKWA** ni **SHULE YA KUTWA** ipo **HALMASHAURI YA JIJI LA DAR ES SALAAM** katika kata ya **BONYOKWA** na mtaa wa **BONYOKWA** umbali ni **MITA 400** kutoka stendi ya daladala ya bonyokwa.

Muhula wa Masomo unaanza tarehe ....................... hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe ......................... Mwisho wa kuripoti ni tarehe ...............................

**2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

**2.1 Sare za Shule**

i. Sare ya shule hii ni sketi 2 (**Dark blue**) kwa Wasichana na suruali 2(**Dark blue**) kwa Wavulana.
**NB. Maelezo ya mshono yameambatanishwa katika ukurasa wa mwisho**
ii. Mashati light blue mikono mirefu (*mawili*);
iii. Rangi ya Hijab (kijuba) ni l i g h t b l u e ; ifunike kifua cha mwanafunzi pia iwe ndefu kufikia kifundo cha mkono akisimama (*ambatisha mshono*);
iv. Sare ya Michezo ni truck ya rangi ya dark blue Kwa wasichana na wavulana
v. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi;
vi. Soksi jozi mbili nyeupe kwa wasichana na nyeusi kwa wavulana;
vii. Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali;
viii. Sweta rangi ya dark blue ;
ix. Tai rangi ya dark blue yenye mistari myeupe.
x. Tisheti (T-shirt); maelekezo yatatolewa baada ya kufika shule.

**2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-**

i) Madaftari (Counter book 4 qiure) idadi ni kulingana na tahasusi;
ii) Vitabu vya masomo ya tahasusi husika.
Iii). English Dictionary;

**2.3 VIFAA KWA MATUMIZI YA SHULE:-**

1. Lete Karatasi za Photocopy **A4 Bunda 1** aina moja wapo kati ya hizi zifuatazo:- **Dolphine** (cover yake rangi ya blue) **TOP COPIE** (cover yake rangi ya kijani).

2. Ruled paper 1 reams, dustless chalks 1 packet.

**a)** Alete vifaa v i f u a t a v y o

(i) Street Broom (chelewa ya kusimama)

(ii) Soft broom 1, squeezer 1

Iii) Spring files 2

Iv) Ndoo kubwa 1

**2.3 Michango mbalimbali**

**Shule za Kutwa**

| Na | na ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | chango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | hadhari | 5,000/= |
| 4. | mbo | 5,000/= |
| 5. | tambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

Lipia ada na michango mingine katika Accounti ya Shule **NMB – ILALA A/**N:- **20310050734** jina la Akaunti ni **Bonyokwa Secondary School.** Malipo yote yalipwe Banki kama ilivyoainishwa kwenye jedwali bila kupungua, **Original Bank Pay Slip** iletwe kwa **Mhasibu** ikiwa na jina la mwanafunzi.

**Nb**: Mzazi/Mlezi atamchangia mwanaye/mwanafunzi chakula cha mchana

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;

ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;

iii. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;

iv. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;

v. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;

vi. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
vii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
viii. Kutunza mali za shule;
ix. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
x. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi; ikikamatwa, simu itavunjwa na kuharibiwa mbele ya wanafunzi wengine.**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:** i. Wizi;

I. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
ii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iii. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
iv. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
v. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vi. Kufuga ndevu;
vii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
viii. Uvutaji wa sigara;
ix. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
x. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xi. Kusababisha mimba;
xii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiii. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xiv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xv. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvi. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xvii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

## 4. Viambatisho na Fomu Muhimu

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na

Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali; ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;

iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na

iv. Picha mbili (2) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi pamoja na Namba zao za Simu.

**5.** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**ZINGATIA:** Unapaswa kuja na fomu zilizoambatanishwa na barua hii zikiwa zimejazwa kikamilifu. Fomu hizi ni viambatanisho **A, B & C.** Pamoja na Cheti cha **kuzaliwa, Leaving Certificate** ya Kidato cha **IV** na **Result Slip** (kila cheti kiwe Original na Photocopy yake.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**Saini ya Mkuu wa Shule ................................**

**Jina la Mkuu wa Shule : Arnold A Tenganamba**

**Mhuri wa Mkuu wa Shule:**




**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa.**

**TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU**

**MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule : 0755865326**
- **Makamu Mkuu wa Shule : 0714057027**
- **Mwandamizi Taaluma : 0714333431**
- **Mwandamizi Malezi : 0714148876**

**KIAMBATANISHO 'A'**

**HALMASHAURI YA JIJI LA DAR ES SALAAM**
**BONYOKWA HIGH SCHOOL**
**FOMU YA KUANDIKISHWA**

**Picha mwanafunzi**

(a) **Ijazwe na mwanafunzi**:

1. Jina kamili la mwanafunzi ______________________________
2. Uraia
   ______________________________
   ______________________________
3. Tarehe ya kuzaliwa ______________ Uzito............Kg ,Urefu...........Cm
4. Namba ya cheti cha kuzaliwa......................................
5. Mkoa aliozaliwa ______________________________
6. Yatima/Siyo yatima______________________________
7. Kata unayoishi______________________________
8. Umbali kati ya unapoishi na Shule ilipo km 3 ☐ zaidi ya km 3 ☐
9. Shule alizosoma kabla ya kuja Sekondari ya Bonyokwa

| JINA LILILOANDIKISHWA SHULENI | SHULE YA MSINGI/ SEKONDARI | TAREHE NA MWAKA ALIOANZIA | TAREHE NA MWAKA ALIOTOKA |
|---|---|---|---|
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |

(b)

**Maelezo binafsi ya mzazi / mlezi**

**Picha mzazi/mlezi**

Jina kamili la Mzazi / Mlezi ______________________________

1. Uraia
   ______________________________
2. Anuani kamili mjini DSM ______________________________
3. Sehemu unayoishi ______________________________
4. Mtaa ______________________________
5. Namba ya nyumba ______________________________
6. Namba ya simu ______________________________(ya haraka)
7. Namba ya NIDA:..............................................................................
8. Jina la Mwajiri na Idara ______________________________
   - Anuani : ______________________________
   - Namba ya simu : ______________________________
   - Kazi ya mzazi / mlezi : ______________________________(Mfano : Karani,

Meneja, Mwalimu n.k.
**Sahihi ya mzazi / mlezi _ ___________________________________**

**KIAMBATANISHO ' B'**

Mkuu wa Shule,
Bonyokwa High School,

S.L.P. 24302,

**DAR ES SALAAM.**

Picha ya Mzazi / Mlezi

**YAH: AHADI YA MZAZI / MLEZI KUKIRI KUKUBALIANA NA SHERIA, KANUNI NA MAELEKEZO YA SHULE**

Mimi ______________________________________________ Mzazi / Mlezi wa mwanafunzi_____________________________________________ wa kidato cha **Tano** katika Shule ya Sekondari ya Bonyokwa, nathibitisha kuwa nakiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo yote ya shule. Naahidi pia kumsimamia mwanafunzi afuate sheria, kanuni na taratibu za shule. Naahidi pia kutoa ushirikiano na shule kwa manufaa ya mwanangu na kulipa ada na michango kwa wakati.

**Jina la Mzazi / Mlezi :** _____________________________________________

**Sahihi ya Mzazi / Mlezi :** ___________________________________________

**Namba ya simu:** ____________________________________________________

**KIAMBATANISHO ‘ C’**

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**PRESIDENT OFFICE – TAMISEMI**
**DAR ES SALAAM CITY COUNCIL**
**STUDENT MEDICAL CERTIFICATE**

To be completed by a Government Medical Officer and returned to be Headmaster of Bonyokwa High School, P. O. Box 24302, DSM.

To the Medical Officer, Date:

__________________________________

__________________________________

**RE:** ________________________________________________________________

Please, examine the student mentioned above and comment on his / her health by responding to the following items. Kindly put a tick or cross in from of either **YES** or **NO** as you find appropriate.

**ARNOLD A TENGANAMBA**
**HEDMASTER**


3. Does the student have problems in connection with:
   (a) Sight? **(1) No** **(2) Yes**
   If yes, state ____________________________________________________
   (b) **Hearing?** **(1) No** **(2) Yes**
   If yes, state ____________________________________________________
   (c) **Speech?** **(1) No** **(2) Yes**
   If yes, state ____________________________________________________
   (d) **T.B?** **(1) No** **(2) Yes**
   If yes, state ____________________________________________________
   (e) **Blood pressure?** **(1) No** **(2) Yes**
   If yes, state ____________________________________________________
   (f) **Any physical disability? (1) No** **(2) Yes**
   If yes state ____________________________________________________

4. Do you, therefore, recommend the said student medically fit for studentship at this School **(1) No (2) Yes. If no, please state reasons**.

   __________________________________________________________

   **Date:** ___________________ **Name & Signature of M. O** _____________________

**Designation & stamp**


MSHONO WA SKETI
ZIP
NYUMA
MBELE.
MSHONO WA SURUARI




2.

RANGI YA KITAMBAA CHA SHULE



